**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE SIKU YA KUINGIZWA KAZINI KWA ASKOFU DKT ALEX GEHAZ MALASUSA KUWA MKUU WA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA (KKKT), TAREHE 21 JANUARI 2024**

*Mhashamu Baba Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT);*

*Mhashamu Askofu Dkt. Fredrick Shoo, Mkuu wa Kanisa mstaafu;*

*Pamoja na wenzi wenu;*

*Mheshimiwa Dkt Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Waheshimiwa Mawaziri mliopo;*

*Katibu Mkuu Kiongozi;*

*Katibu wa Chama cha Mapinduzi na Viongozi wenu wa Vyama vya Siasa;*

*Mama Anna Mkapa,*

*Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mhashamu Askofu Johannes Ole Meliyo, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Kenya (KELC);*

*Mpendwa Askofu Dkt. Christian Samraj, wa Kanisa la Kilutheri la India Kusini;*

*Mhashamu Askofu Dkt Yonas Dibisa – Makamu wa Rais wa Shirikisho la Makanisa ya Kilutheri Duniani (Lutheran World Federation);*

*Mpendwa Mch. Dkt. Fidon Mwombeki, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Barani Afrika (All Africa Conference of Churches) (AACC);*

*Wahashamu Maaskofu wote wa KKKT na Maaskofu wa Makanisa mengine mliopo pamoja nasi;*

*Wapendwa Maaskofu na Viongozi wengine wa dini;*

*Wanachama wa Umoja wa Kiinjili wa Misioni (UEM);*

*Waheshimiwa Wasaidizi wa Maaskofu;*

*Wapendwa Makatibu Wakuu wa KKKT na CCT pamoja na Makatibu Wakuu wengine mliopo;*

*Mheshimiwa Mufti pamoja na Viongozi Wakuu wa Dini mliopo;,*

*Waheshimiwa Mawaziri;*

*Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;*

*Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Waheshimiwa Wabunge mliopo;*

*Waheshimiwa Viongozi wa Serikali;*

*Wageni waalikwa wenzangu;*

*Washirika;*

*Waandishi wa habari;*

*Mabibi na Mabwana:*

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…!***

***Bwana Yesu asifiwe sana…!***

## Utangulizi

***Ndugu wana KKKT,***

Maneno matakatifu ya Biblia, katika Kitabu cha Mathayo **Sura ya 11, Mstari wa 20** yanasema *"**Kwa maana popote pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu, mimi nipo hapo kati yao**"*. Katika mkusanyiko huu wa kumuombea Kiongozi wetu aliyeitwa na kuitika wito wa kulitumikia Kanisa, hatuko pekee yetu; Bwana Mungu yu pamoja nasi. Hivyo, tunayo kila sababu ya kumshukuru na kumtukuza Mungu kwa rehema zake zisizokoma kwa kutuwezesha kushuhudia ukuu wake leo hii kupitia tukio hili adhimu katika Kanisa la KKKT.

Bado ninayo kumbukumbu nzuri sana ya sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya KKKT zilizofanyika mjini Arusha mwezi Agosti mwaka 2023. Mwaliko wenu huu wa kutaka nijumuike nanyi tena katika tukio hili la kihistoria katika

utumishi wa Askofu Dkt Alex Gehaz Malasusa, umedhihirisha upendo wa kipekee kwangu binafsi na kwa Serikali ninayoiongoza. ***Ahsanteni sana!***

Nitumie fursa hii pia kama Mkuu wa Nchi, kuwakaribisha sana wageni wote waliotoka nje ya nchi ili kushuhudia tukio hili kubwa hapa nchini. Karibuni sana. *Distinguished guests we warmly welcome you all to Tanzania. We are honoured and blessed to have you with us and it is our hope that you will enjoy your stay. You are welcome to Tanzania.* Uwepo wa wageni hawa ni uthibitisho na kielelezo tosha cha mapenzi yaliyopo kwa KKKT na ushirikiano walioujenga na kuudumisha baina yao na Taasisi zingine na waumini kwa jumla. ***Hongereni sana!***

## Pongezi

***Mhashamu Askofu Malasusa,***

Ninakumbuka mara tu ulipochaguliwa kuliongoza Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), nilikuandika kupitia mtandao wa kijamii kukutakia kheri na kukutia moyo. Mimi sikukuuliza kama uko karibu na Serikali, lakini nilikutia moyo. Nilirejea maneno ya Biblia Takatifu, kwenye Kitabu cha Kumbukumbu la Torati, Sura ya 31 Mstari wa 8 yasemayo:

***"Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike".*** Nilitumia hekima ya maneno hayo kwa kutambua uzito wa majukumu ya uongozi na dhima unayoibeba kwa Mungu na kwa waumini wa Kanisa hili.

Kwa sie tulio kwenye uongozi, pamoja na kukupa hongera pia ni lazima tukupe pole na kukuombea subra, hekima na stahamala kwenye uongozi wako. Uwezo; uzoefu na kujituma kwako kumekuvusha mpaka kufikia hatua hii tunayoishuhudia leo hii. Natambua penye nia hapakosi njia, na kama hapana njia, basi Bwana atafanya njia. Niombe ukawe baraka kwa Kanisa hili; waumini na Taifa kwa ujumla.

Baba Askofu, ninatambua kwamba, pamoja na kuwa muumini mzuri na msomi hodari wa Theolojia, uliwahi pia kuwa Mkuu wa KKKT kati ya mwaka 2007 hadi 2015, pale ulipopokea kijiti kutoka kwa Askofu Dkt. Samson Mushemba, Mwenyezi Mungu amrehemu. Ninatambua pia kuwa, ulikuwa Mkuu wa KKKT wa kwanza mwenye umri mdogo kuliko wote kuwahi kuliongoza Kanisa hili, ukiwa na umri wa miaka 47 tu. Hivyo basi, kuchaguliwa kwako leo kwa mara nyingine hakujaja kwa bahati mbaya, bali kumetokana na historia yako

na ukomavu katika uongozi wa Kanisa. Aidha, kunadhihirisha imani ya viongozi na waumini wenzako waliyonayo juu yako. ***Hongera sana Baba Askofu.***

Ni dhahiri kwamba, unao uzoefu, uwezo na uelewa mkubwa kuhusu misingi pamoja na mifumo ya uendeshaji wa Kanisa hili. Hivyo, waumini wa Kanisa hili na wananchi kwa ujumla watanufaika sana na ubobezi wako. Ninatambua wewe ni mtu wa maombi na mwepesi wa kujifunza kutoka kwa wengine. Kwa hivyo, unapopokea majukumu haya, ningependa kukushirikisha maneno mazuri kutoka Kitabu cha Mithali Sura ya 3, Mstari wa 5 na 6, yasemayo, *"**Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyoosha mapito yak**o."*

Kwa niaba ya Serikali, ninapenda kukuahidi ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa wito huu mkuu na katika majukumu yako. Kwa waumini wa KKKT na Watanzania wote kwa ujumla, nawasihi wakuunge mkono na kukuombea ili uendelee kuliongoza Kanisa hili kwa mapenzi na uaminifu mkubwa kama ambavyo umekuwa ukifanya.

## Shukrani kwa Askofu Dkt Shoo

***Ndugu zangu wana KKKT,***

Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza mtangulizi wa Baba Askofu Malasusa naye ni *Mhashamu Baba Askofu Dkt. Fredrick Shoo.* Chini ya uongozi wake alifanya jitihada za kuendelea kuiimarisha KKKT na leo hii anakukabidhi Kanisa lililo imara zaidi, na lenye mchango mkubwa kwa waumini na Taifa kwa ujumla. Namshukuru sana Askofu Dkt Shoo kwa ushirikiano wake kwa Serikali ninayoiongoza.

Ninataka niseme hapa mbele yenu waumini, nilikuwa ninalisikia Kanisa la KKKT, lakini kaka yangu Dkt Shoo ndio amelitambulisha Kanisa hili kwangu na nikalielewa vizuri sana. Ni imani yangu kuwa milango yake itaendelea kuwa wazi na mikono yake itaendelea kutupokea tutakapohitaji kuchota kwenye kisima chake cha hekima na busara ambacho Mungu amempa yeye.

**Risala ya Askofu Malasusa**

***Baba Askofu Malasusa,***

Nimeisikiliza hotuba yako kwa umakini, imeelezea mambo mengi ya msingi na ya kiuongozi. Kwa ufupi, umezungumzia **umoja, amani na mshikamano wa kitaifa. Lakini pia umezungumzia uchaguzi wa Serikali za Mitaa.**

Kuhusu **amani**, nami nakubaliana nawe kwa asilimia mia moja, kwamba tukiwa wamoja, tutajenga Taifa lenye umoja, mshikamano na lenye watu wanaoheshimiana na kuthaminiana. Kama ambavyo umoja ni muhimu kwa Kanisa, vivyo hivyo, umoja ni muhimu zaidi katika ujenzi wa Taifa. Maneno haya nimemsikia akiyasema vizuri sana Mhashamu Baba Askofu (*Dkt. Christian Samraj*) kutoka India. Ninamshukuru sana na mimi ninaungana naye.

Katika kuyatia nguvu maneno haya, katika uongozi huu, tumekuja na falsafa ya R nne yaani *maridhiano, mageuzi, ustahimilivu na kujenga upya.* Ninataka kuzihusisha R nne na maneno yaliyosemwa kwenye Kitabu cha Marko, Sura ya 3, Mstari wa 25, yanayosema, ***"Nayo nyumba kama ikigawanyika dhidi yake yenyewe, nyumba hiyo haiwezi kusimama".*** Huku

Waswahili tunasema, ***'nyumba isiyolongwa haimei'.*** Yaani nyumba ikiwa na tofauti ambazo hazizungumzwi, nyumba hiyo haiwezi kusimama. Nyumba ikigawanyika ndani yake yenyewe hiyo nyumba haiwezi kusimama. Nchi yetu haitakiwi kuwa nyumba ya aina hiyo. Ndio maana tumekuja na falsafa hii ya R nne, ambayo inatuasa kuwa ili tuweze kupiga hatua kubwa za kimaendeleo ni lazima tuendelee kuwa wamoja kwa kuhubiri na kuishi kwa umoja. Haya yote hayaji bila kuwepo na mazungumzo, kama alivyosema Baba Askofu Malasusa.

Mhashamu Baba Askofu, umezungumzia pia suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Binafsi ninauchukulia uchaguzi huu kwa uzito mkubwa sana, kwani ni uchaguzi unaotoa uongozi katika maeneo tunayoishi. Nirejee wito wangu kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye uchaguzi huo, na kwa vyama vya siasa, viteue wagombea wazuri ili wananchi wawe na uwanja mpana wa kuchagua viongozi wanaowafaa. Hakika, dhamira yetu ya kuimarisha demokrasia iko wazi na hilo tunaendelea kulisimamia.

Hata hivyo, kama wasemavyo wataalam wa demokrasia, ujenzi wa demokrasia unahitaji zaidi ***wanademokrasia,*** pengine kuliko hata demokrasia yenyewe. Kujenga demokrasia

sio tu kuwepo kwa demokrasia, lakini pia kunahitajika wanademokrasia kuijenga hiyo demokrasia yenyewe. Kwa bahati mbaya, sio kila aliye kwenye michakato ya kidemokrasia ni mwanademokrasia. Wengine ni wanaharakati. Hapa ndipo tunapopata shida: kutofautisha uanademokrasia na uanaharakati. Hata hivyo, tutaendelea kulinda na kudumisha misingi ya demokrasia hapa nchini kwetu, na kuhakikisha kuwa tunaweka mazingira yatayowezesha demokrasia kushamiri zaidi huku tukiendelea kulinda amani na umoja wa kitaifa.

Ni kweli kwamba, amani ni kichocheo kikubwa cha maendeleo na ustawi wetu. Serikali itaendelea kutunza amani ya nchi yetu, ili wananchi waendelee na shughuli zao mbalimbali za ujenzi wa Taifa ikiwemo kutekeleza haki yao ya kuabudu. Utakumbuka mwezi Agosti 2023 kwenye maadhimisho ya miaka 60 ya Kanisa hili, nilirudia mara tatu tena kwa msisitizo mkubwa, kwamba, **hakuna mwenye misuli wala ubavu wa kuharibu amani na usalama uliojengeka kwa miaka mingi kwenye Taifa hili.** Serikali itasimamia kwa nguvu zote uwepo wa amani na usalama, tukiongozwa na hekima na busara pia. Niwahakikishie Watanzania wote

kwamba, Tanzania ni salama na ni wajibu wetu Serikali kuendelea kudumisha amani na usalama huo.

## Ujumbe maalum kwa Taasisi za dini

***Ndugu zangu wana KKKT,***

Niruhusuni nizungumzie sasa suala moja lenye umuhimu wa kipekee kwangu binafsi kama mwanajamii na kiongozi wa Serikali. Suala linalohitaji ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na Taasisi zote za dini nchini. Hili si jambo jingine bali ni **umuhimu wa kudumisha taasisi ya familia nchini** (*protection of the family unit*).

Katika hili, ningependa kujielekeza katika masuala mahususi matatu: **kwanza** kuhusu changamoto katika kulinda familia; **pili** kuhusu madhara yake kwa ustawi wa jamii; na **tatu na mwisho** ni kuhusu nafasi za taasisi za dini katika kulinda familia.

***Ndugu zangu,***

Taasisi ya familia kote ulimwenguni na hapa nchini, inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Ripoti ya Utafiti wa Ufuatiliaji wa Kaya ya 2020/2022 ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaonesha kwamba, zaidi ya nusu ya watanzania

walio katika umri wa kuoa au kuolewa, hawajaingia kwenye ndoa. Kwa wakazi wa mijini ni wastani wa 61.5% wakati vijijini ni 55.5%.

Aidha, kwa wale wanaofanikiwa kuingia kwenye ndoa, kuna changamoto mbalimbali zinazosababisha migogoro ya ndoa. Kwa mfano, mwaka 2022/23 tulikuwa na mashauri ya migogoro ya ndoa **39,571**. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24 pekee, tayari tumepokea mashauri **28,773**. Kwa upande mmoja, ongezeko hili limetokana na kuboreshwa kwa mfumo wa kuripoti na uamuzi wa kuajiri Maafisa Ustawi wa Jamii zaidi.

Jambo hili inabidi tulitafakari kwa kina kama wanajamii, kwani asilimia kubwa ya migogoro hii ya ndoa inahusisha ndoa za vijana, au ndoa changa. Tunatoa fedha nyingi, harusi kubwa, michango mingi, lakini baada ya mwaka au miaka miwili, watoto kila mtu anarudi kwake. Sasa wazazi tuna wajibu wa kuhakikisha taasisi hii ya familia inapewa umuhimu wake.

Kwa upande mwingine, familia zetu pia zinakabiliwa na changamoto ya matukio ya ukatili. Kwa mujibu wa takwimu za

Jeshi la Polisi, mwaka 2022 kulikuwa na matukio ya ukatili **30,566** yakilinganishwa na matukio **29,373** yaliyoripotiwa mwaka 2021, hili ni ongezeko la **4.1%.** Takwimu hizi zinaonesha waathirika wakubwa wa matukio ya ukatili ni wanawake na watoto. Hali hii ni lazima ibadilike kama kweli tunapata mafunzo ya kiimani.

Hapa kuna swali kubwa, na kuna kazi kubwa ya kufanywa baina ya Serikali na viongozi wa dini. Inatakiwa kazi ya wokovu wa roho za watu. Haya yanafanyika kwa sababu roho za watu zimeharibika. Tunaishi kama kwenye ile hadithi ya *the Animal Farm,* kila mmoja anamuwinda mwenzake. Tukiangalia wingi wa Taasisi za dini na matokeo haya, haviendani. Lazima tujitafakari kama wanajamii, nafasi yetu kama Taasisi za Dini, nafasi ya Serikali na wajibu wa jamii yenyewe. Tunafanyaje kulinda dhidi ya haya yanayotokea.

Wataalam wanasema, *family is the basic unit of a society,* yaani familia ni taasisi ya msingi kwa jamii yoyote. Bila familia hakuna jamii, na bila jamii hakuna Taifa. Kama familia zinaharibika inamaanisha jamii yetu itakuwa ya ovyo na kama jamii ni ya ovyo, Taifa litakuaje?. Lazima tujitathmini, tuangalie tumejikwaa wapi, na turekebishe ili tujenge Taifa bora.

Athari za kuvunjika kwa familia ni kubwa sana na zinajidhihirisha kwenye jamii yetu. Vitendo vya ukatili na athari katika malezi ya watoto ni sehemu tu ya matokeo ya kuitikisa taasisi ya familia. Tunashuhudia ongezeko la watoto wanaokosa misingi ya malezi ya familia na kuongeza hatari ya kulelewa na watu wasio na nia njema kama anayoweza kuwa nayo mzazi kwa mwanaye.

Mzazi unapomlea mwanao, unamlea kwa mapenzi yote, ili awe mtoto mwema, akufae na alifae Taifa. Baba ukitoa talaka kwa mama na kwa watoto pia, watoto wanaenda kulelewa na mama asiye na uwezo na kipato, watoto wanakuwa wenyewe na wanalelewa na watu huko njiani. Matokeo yake tunazalisha watoto wenye majina kadhaa. Watoto wetu tunawaita ″panya road″ mara ″mbwa mwitu″ watoto wetu wenyewe wana majina ya ajabu.

Watoto wengine wanaobahatika kupita shule vizuri na wakakua wakawa vizuri, lakini wamekosa msingi mzuri wa malezi ya familia na ya kidini, utendaji (*performance)* wao pia unakuwa wa ajabu. Kwa hiyo kama kweli tunataka kujenga Taifa zuri la Tanzania kama Mungu alivyoliumba vizuri, Mwenyezi Mungu ameliumba Taifa zuri (mito, mabonde, ardhi

nzuri, bahari, watu wazuri, nyoyo rahimu) ninaomba sana viongozi wa dini tushirikiane na Serikali tuone tumekosea wapi na tujenge vizuri Taifa letu.

Kwa kutambua changamoto hii na athari zake kwa jamii, mwaka 2022, tuliamua kuunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa lengo la kushughulikia changamoto na kutoa huduma kwa makundi maalumu yakiwemo watoto, wanawake na wazee. Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Maafisa Ustawi wa Jamii kote nchini, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Natambua, bado hawatoshi, lakini tutaendelea kuimarisha kadri hali inavyoruhusu na tutashirikiana na wadau wengine katika kuhakikisha huduma hizi zinapatikana.

Tutaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari hasi zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi yasiyofaa ya mitandao ya kijamii. Ninadhani huyu ni adui mkubwa wazazi wenzangu. Kwa hiyo, wazazi tuwe makini katika kuwachunga watoto wetu na simu na mitandao ya jamii.

Pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado suala hili linahitaji ushirikiano zaidi. Ndio maana nilidhani, ujumbe

wangu wa siku ya leo ujikite katika suala la familia na malezi. Ninaamini Taasisi za dini zina nafasi kubwa ya kusaidia kwa kutoa mafundisho ya ndoa na familia.

Nilikuwa ninazungumza na Makatibu hapa wakati kwaya zikitumbuiza, kila kwaya zikija wanawake ni wengi kuliko wanaume. Wakaniambia hata kwenye mafundisho wanawake ni wengi kuliko wanaume. Waliniambia pia kuna kwaya ya wenza wa wachungaji, wanawake. Nikauliza endapo kuna kwaya ya wenza wa wachungaji wanawake, wakanijibu, hapana. Sasa, oneni jinsi wanaume mnavyoliacha Kanisa. Wanawake ndio tumebeba Kanisa, ndio tumebeba dini. Watoto wanakuja kupata kipaimara, kisha komunio, wote wa kike na wa kiume, je, wanaume wanaishia wapi?

Ujumbe wangu hapa ni kwamba, tukamate watoto wetu waje kanisani. Wapate mafunzo ya dini, watoto wa kike na watoto wa kiume. Kwa dini nyingine hivyohivyo, tuhakikishe watoto wetu wa kiume na wa kike wote wanapata mafunzo ya dini ipasavyo. Kwa sababu ni kupitia dini tu ndio tunapata miongozo ya maisha. Tungekuwa wote tumepata miongozo ya maisha, mengi ya yanayotokea sasa yasingetokea.

Ninataka nihusishe nilichosema na Kitabu cha Wakolosai, Sura ya 3 mstari wa 18 hadi 20, kuhusu wajibu wetu kwa familia na malezi yanayofaa. Naomba ninukuu *'**Ninyi wake, watiini waume zenu kama inavyopasa katika Bwana; Ninyi waume, wapendeni wake zenu wala msiwe wakali juu yao; Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote, kwa maana hii humpendeza Bwana; Ninyi akina baba msiwachokoze watoto wenu wasije wakakata tamaa'**.*

Kama maandiko yanatuelekeza hivi, si wote tunavyo hivi vitabu, twendeni tukasome tena hiki kipande. Halafu kila mtu ajitathmini mwenyewe, je yaliyoandikwa hapa yapo ndani ya nyumba yake?**.** Ni muhimu sana kuimarisha taasisi ya familia, kwani familia ikiwa imara na yenye masikilizano, itatoa malezi mema kwa mtoto na itaandaa muumini mwema, wanajamii wema, na raia wema. Raia mwema aliyetokana na malezi mema, atakuwa ni kiongozi mzuri na anayo nafasi kubwa zaidi ya kulea raia wengine wengi wa aina yake. Hapo ndio Taifa litakuwa limesimama vyema.

Hivyo, Taasisi za dini zina mchango mkubwa katika kufinyanga Taifa lenye watu wema na wanaowajibika. Tunayopambana nayo leo mengine yanatokana na kutopata

maadili ya dini. Walijilea wenyewe na kwa hiyo wanajiendea tu. Lakini sasa turudi, tujirekebishe, makosa yale tuliyoyafanya sasa tusiyafanye tena.

**Mvua kubwa katika baadhi ya Mikoa**

**Ndugu zangu,**

Baada ya kusema hayo, ninataka kugusia kidogo masuala ya hali hewa tunayoipitia sasa. Mtakumbuka Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) ilitoa tahadhari kuhusu mvua kubwa katika baadhi ya maeneo yetu Tanzania. Tumepata taarifa na tumejionea athari zinazoendelea kuripotiwa au kutolewa taarifa kutokana na mvua hizo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ikiwemo vifo na kuharibika kwa miundombinu na kukatika kwa mawasiliano.

Nitumie fursa hii, kwanza kutoa pole kwa wananchi wenzetu waliothirika na mvua hizi na niwaombe sote tuwakumbuke kwa sala, maombi na majitoleo ili tuwasaidie na wao waweze kuishi vyema.

Kwa upande wetu Serikali, tayari tumewaelekeza Mawaziri wa kisekta kama Ujenzi, Afya, Maji na Umeme, kwamba wakae kwa tahadhari na wachukue hatua za haraka

pale matatizo yanapotokea. Nimeelekeza Mamlaka zote kuwa kwenye hali ya tahadhari na utayari, na Jeshi la Uokoji lijipange kutoa msaada wa haraka.

Ndugu zangu, pamoja na Serikali kuwa tayari, kwa miaka mingi tumekuwa tukizuia wananchi kujenga kwenye maeneo hatarishi. Pamoja na wito huo, bado baadhi wamejenga pembezoni mwa mito na kwenye maeneo hatarishi. Tumekuwa tukizungumzia masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo tunawataka wananchi wawe na hadhari. Wale wanaojua wapo kwenye maeneo ya hatari waondoke, wasogee juu.

Hatuwezi kudhibiti kiwango cha mvua kinachonyesha. Kwa vijijini tumeanza kuchimba mabwawa ya kuhifadhi maji, tumeweza kutengeneza catchment areas (maeneo ambayo yatadaka maji) na kuyapeleka kwenye mabwawa mbalimbali kwa mifugo, kilimo na umeme. Katika maeneo ya miji, hayo hayawezi kufanyika. Niombe sana wananchi, tuchukue tahadhari, na kuliepusha Taifa na misiba mikubwa au hatari kubwa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Leo nimepata nafasi ya kuzungumza na wananchi, nilidhani ni vizuri nilizungumze hili. Niwaombe sana wananchi wasikilize yale tunayoyasema na wachukue hatua.

## Hitimisho

***Ndugu zangu,***

Nikihitimisha hotuba yangu, naomba nimpongeze tena Mkuu wetu mpya wa KKKT na kumtakia kila la heri.

Ninamuahidi yeye na viongozi wote wa dini nchini kwamba, Serikali yangu itaendelea kulinda uhuru wa kuabudu nchini kama ulivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Niwashukuru tena kwa mwaliko ambao umenipa fursa leo ya kuzungumza na Taifa.

Ninashukuru zaidi kwa mapokezi mazuri, na kwa zawadi mliyonipatia. Nawatakieni nyote neema na Baraka za Mwenyezi Mungu.

Kwa kaka yangu Malasusa, ninakutakia Utumishi mwema! Kwa kaka yangu Fredrick Shoo ninakutakia utumishi mwema kwenye Dayosisi yako. Mwenyezi Mungu awabariki wote.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**